Maishani mwangu niliamini; unyenyekevu na heshima vinaweza kuwa dira kwa mwanaume nimpendaye.

Niliamini itakuwa kinga ya kudumisha mahusiano, na kufikia hatua nzuri, ile ibarikiwayo kwa utunuku wa cheti. Na uhalalisho toka kwa Mwenyezi Mungu.

Hakika! Pasi na chembe ya shaka. Au imani, nilidiriki kumkabidhi hisia zangu kwa asilimia zote. Kiasi cha kutokuwa msikivu kwa lolote baya nisikialo juu yake.

Sikuwa na budi kujivika utumwa wa upendo. Naweza sema hivyo, kwa ajili ya kutunza yangu siha. Na kuhimarisha uhusiano, huku nikisahau, u-hawara, haupaswi kuwa na majivuno.

Lakini mimi nilijivunia.

Kitendo kilichopelekea kujihalalishia mateso ambayo ni ngumu pasi na kuyaachia historia yenye kumbukumbu.

Nimeamua kushirikiana nawe katika kumbukizi hizi. Ili usipitie makosa ambayo nimepitia. **SONGA NAYO UNONOKE...**

**NENDA.**

Ni riwaya iliyobeba hisia za kijana wa kiume na kuwasilishwa na kijana wa kike.

Yumkini unajiuliza, kwa nini aende?

Yupi ambaye ruksa aondoke maishani mwako?

Tena aondoke pasi na kumbukizi zozote zinazokuhusu?

Nawe usipate maumivu ya aina yoyote juu ya kuondoka kwake?

Kisa hiki kinakufumbulia maswali haya.

Riwaya iliyosheheni visa vilivyosukwa kwa umakini na mpangilio wenye kukutekenyesha kufahamu lijalo.

*Njoo tuburudike. Njoo tuelimike.*

TANURU LA SIMULIZI

*Burudisho maridhawa la moyo wako.*

*"Kwenye maisha hakuna jaribio. Kila lifanywalo, hufanywa kwa mpangilio ulioamuliwa kwa utimamu wa akili."* HASSANI MBONECHE.